Appendix 3.

Dondoo za Ufugaji Bora Kuku wa Asili

Muhtasari wa ufugaji kuku wa asili ili kuzuia vifo na kuboresha uzalishaji

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE
1984
AROHI NI HAZINA

wellcome trust

Yaliyomo

Dondoo ya 1.Usafi wa vyombo na mazingira ya kuku 1
Dondoo ya 2. Magonjwa na kinga kwa kuku wote 2
Dondoo ya 3 .Chakula cha ziada 3
Dondoo ya 4. Utotoleshaji wa vifaranga 4
Dondoo ya 5. Matunzo ya vifaranga kuzuia vifo 6

Utangulizi

Ufugaji wa kuku wa asili ni nyenzo muhimu katika kupambana na lindi la umasikini kwa kuongeza kipato cha kaya. Hata hivyo pamoja na soko la uhakika, bado ufugaji kuku haujaweza kutumika ipasavyo kupambana na umasikini unaowakabili watanzania wengi. Ni mazoea kwa jamii nyingi hapa Tanzania kufuga kuku wa asili kama sehemu ya mila na desturi zao. Kuku wa asili amekuwa akifugwa bila kupatiwa huduma muhimu kama; makazi bora, chakula cha ziada, tiba na kinga za magonjwa mbalimbali. Muhtasari huu unatoa muongozo wa ufugaji kuku wa asili ili uweze kuzalisha na hatimaye kuuza kuku kwa wingi.

*Dondoo ya 1.*Usafi wa vyombo na mazingira ya kuku

Uchafu ni mama wa magonjwa hivyo zingatia haya;

1. Vyombo vya chakula na maji visafishwe mara kwa mara kwa maji na sabuni.
2. Pumba au chakula kilicholowana na kuchanganyika na kinyesi cha kuku vitolewe na kuzikwa.
3. Choma moto au zika kwenye shimo refu kuku waliokufa kwa ugonjwa.
4. Usifuge kuku na ndege wa jamii nyingine kwa mfano bata katika banda moja.

5. Ondoa mbolea mara kwa mara kutoka katika banda la kuku.
6. Tumia dawa za kuulia vimelea kusafishia banda na upake chokaa banda angalao mara moja kwa mwaka.
7. Ziba matundu yote yanayoweza kuruhusu panya na wanyama wakali kama vicheche kuingia katika banda la kuku

Dondoo ya 2. **Magonjwa na kinga kwa kuku wote**

- **Ndui ya kuku**

Huathiri sana vifaranga wanaokua na hujitokeza kwa wingi wakati wa mvua ndefu. Husababisha vivimbe katika uso, kishungi na hata sehemu nyingine zisizo na manyoya.

- **Mdondo/Kideri**

Mdondo, au kwa majina mengine Lufuo, au kideri ni ugonjwa hatari kuliko yote kati ya magonjwa ya kuku wa asili. Ni ugonjwa wa virusi ambao huathiri kuku wa rika zote, huweza kuangamiza kuku wote kijijini.

- **Ukosefu wa vitamini 'A'**

Ugonjwa huu husababisha macho kuvimba na kutoa uchafu mzito (angalia picha)kama sabuni iliyolowana. Kuku wenye dalili hizi hawaponi na hatimaye hufa. Ugonjwa hujitokeza baada ya kipindi kirefu cha kiangazi kwa ajili ya ukosefu wa majani mabichi.

- **Koksidiosisi**

Huathiri kuku wa umri wowote lakini huua zaidi vifaranga na kuku wanaokua. Kuku hudhoofika, manyoya huvurugika na kuku huwa kama amevaa koti. Kuku huharisha damu au kinyesi cha kahawia na huzubaa na kuonekana kama amevaa koti

- **Viroboto, chawa na utitiri**

Hawa ni wadudu wa nje wanaoshambulia ngozi. Huweza kusababisha ugonjwa kutokana na kunyonya damu.Viroboto hushambulia kichwa na kunata huku vikinyonya damu. Viroboto huua vifaranga. Chawa na utitiri hughasi kuku hadi wakashindwa kutaga na kuatamia.

- **Minyoo**

Minyoo huweza kudhoofisha kuku na kuwafanya waweze kuugua maradhi mengine kirahisi. Muone mtaalamu ukihisi kuku wako wana minyoo.

Jedwali: Linaainisha utaratibu wa kinga za magonjwa ya kuku.

UGONJWA	JINSI YA KUUDHIBITI
Mdonde	Chanja kuku kila baada ya miezi mitatu. Pata chanjo kutoka ofisi za mifugo au maduka ya dawa za mifugo. Chanjo huuzwa katika dozi ya kuku 400 au 1000. Kuna chanjo inayostahimili joto ambayo hutolewa kwa matone au unaweza kutumia chanjo ya 'La Sota' ya kunywesha katika maji. Wafugaji waunde vikundi vya ushirika wa kuchanja kuku ili kupunguza gharama za ununuzi.
Ndui	Chanjo hutolewa kwa njia ya sindano na itolewe na mtaalamu wa mifugo kabla ya mvua ndefu kuanza.
Ukosefu wa vitamini A	Watafutie kuku majani mabichi au hata mchicha mara kwa mara. Kama hakuna majani wape vitamini ya kuku kutoka dukani kama ziada.
Koksidiosisi	Safisha banda kila siku na hakikisha hakuna unyevu sakafuni. Wapatie kuku dawa za kinga ya koksidiosisi Amprolium® au salfa kwa siku 3 mfululizo mara wafikishapo umri wa siku 7.
Viroboto, chawa na utitiri	Mwaga majivu katika banda na hasa kwenye viota vya kutagia ili kukinga wadudu.Tumia dawa za dukani mfano 'AKHERI POWDER' na 'SEVIN DUST'kumwagia kuku mwilini na katika mazingira. Paka mafuta ya taa kwa kutumia unyoya wa kuku kwenye viroboto vinavyoonekana.
Minyoo	Wape kuku dawa za minyoo kila baada ya miezi 6.

Chanjo ya mdonde ya matone ni rahisi kutumia.

Chanjo ya ndui hutolewa kwa sindano, muone mtaalamu wa mifugo akusaidie.



***Dondoo ya 3 .*Chakula cha ziada**

- Wapatie vifaranga nyongeza ya protini kwa kuwachanganyia vumbi la dagaa au vichwa vya dagaa vilivyotwangwa kwenye pumba za mahindi.
- Changanya kikombe kimoja cha vumbi la dagaa na vikombe vitano vya pumba za mahindi (tumia kikombe kidogo cha chai).
- Mchwa na wadudu wengine waweza kutumika kama nyongeza ya protini.

- Vuna mchwa kwenye vichuguu au tengeneza mchwa katika njia za mchwa.
- Kutengeneza mchwa: Changanya kinyesi cha ng'ombe na majani makavu, mabua ya mahindi au maranda ya mbao katika chungu au ndoo ya zamani.
- Mwagia maji hadi kila kilichomo kilowane kisha weka katika chombo kama chungu au ndoo. Weka chombo chako katika njia ya mchwa ukikigeuza juu chini na usubiri hadi kesho yake asubuhi, kisha beba vyote vilivyomo na uwamwagie kuku mahali walipo

Dondoo ya 4. Utotoleshaji wa vifaranga

Chagua jogoo bora na tetea bora kuzalisha kuku

Sifa za jogoo bora

- Awe na umbo kubwa, awe na ukiko mzuri na usioangukia upande mmoja.
- Apende kuwa na himaya yake. Ukimpata jogoo mwenye sifa hizi muweke yeye na mitetea 10. Hivyo ukiwa na mitetea 20, jogoo wawili wanatosha.

Sifa za tetea bora

- Tetea bora ni yule mwenye umbo kubwa, uwezo wa kutaga mayai ya kutosha, kuatamia na hatimaye kutotoa vifaranga na uwezo wa kuvilea.

Uhifadhi wa mayai

1.Weka mayai mahali safi na penye hewa ya kutosha.

2. Tumia boksi lililokatwa na kujazwa mchanga mkavu na safi au kasha la kuhifadhia mayai.

3. Weka sehemu butu ya yai iwe upande wa juu na ile iliyochongoka itizame chini.



4. Andika namba au tarehe katika yai siku lilipotagwa

5. Mayai yakishatagwa yatolewe na kuhifadhiwa na moja liachwe kwenye kiota ili kumuita kuku kuja kutaga kesho yake.

Kuatamiza mayai

- Kuku awekewe mayai atakayokuwa na uwezo wa kuyaatamia na kuyatotoa yote.
- Mayai 10 hadi 12 yanatosha kuatamiza.
- Mayai ya kuatamiza yasizidi wiki mbili toka kutagwa.
- Yai la mwisho kutagwa liwe la kwanza kuchaguliwa hadi yapatikane mayai 10 mpaka 12, na apewe kuku kuyaatamia.
- Mayai ya kuatamiza yasafishwe kwa kitambaa kikavu na safi au kilichowekwa spiriti.

Kutotolesha vifaranga wengi kwa wakati mmoja

Kama unataka kuku zaidi ya mmoja waatamie na kutotoa kwa mpigo fanya yafuatayo;

- Kuku wa kwanza akianza kuatamia muwekee mayai viza au mayai yasiyo na mbegu mfano mayai ya kuku wa kisasa au kuku asiye na Jogoo.
- Rudia zoezi hilo hadi utakapofikisha kuku watano kisha wawekee kuku wote mayai yenye mbegu.

***Dondoo ya 5*. Matunzo ya vifaranga ili kuzuia vifo**

Vifaranga wengi hufa kabla ya kufikisha miezi miwili kutokana na magonjwa, baridi na kuliwa na wanyama wengine. Ili kupunguza vifo vya vifaranga wa siku 1 hadi miezi miwili zingatia yafuatayo;

- **Ulinzi dhidi ya mwewe na wanyama wengine**



Weka vifaranga kwenye tenga na kuwafunika ili wasiende mbali wakati wa mchana. wape maji na chakula. Hakikisha hawapigwi jua wala kunyeshewa mvua. Wakati wa usiku walale na mama yao.

- **Chanjo ya Mdondo Kideri/Lufuo**

Kama tetea alichanjwa kabla ya kuanza kutaga vifaranga wanaoanguliwa huwa na kinga ya mdondo ya kuwatosha kwa wiki tatu za kwanza za maisha yao. Wachanje vifaranga hawa dhidi ya mdondo wafikishapo umri wa siku 18.

Vifaranga ambao historia ya chanjo ya mama haijulikani, wapewe chanjo ya mdondo siku ya 3 baada ya kuanguliwa, rudia wakifikisha wiki 3, kisha uchanje kila baada ya miezi 3.

- **Kinga dhidi ya koksidiosisi**

Kinga ya koksidiosisi kwa vifaranga itolewe hata kama ugonjwa haujajitokeza.

- Wape dawa ya *Amprolium*® kwa muda wa siku 3 mfululizo mara wafikishapo siku 7 tokea waanguliwe kama kinga ya koksidiosisi.
- Dawa inaweza kutolewa hata kama wamevuka umri huo. Fuata maelekezo ya mtaalamu juu ya kiasi cha dawa kinachopaswa kuchanganywa katika maji au pumba.
- Kama vifaranga wadogo wataonyesha dalili za kuzubaa kama kuvaa koti wapewe dawa ya *Amprolium*® kwenye maji kwa utaratibu ufuatao; Dawa siku 3 mfululizo: Usiwape kwa siku 2: Dawa tena kwa siku 3.

Hitimisho

1. Hakikisha banda na vyombo vya chakula cha kuku ni visafi kuepusha magonjwa.
2. Usichanganye kuku na bata katika banda moja.
3. Lisha chakula cha ziada hasa kwa vifaranga.

4. Kideri, koksidiosisi, ndui na upungufu wa vitamini A ni vyanzo vikuu vya vifo kwa kuku wako. Kumbuka kukinga kuku wako dhidi ya magonjwa haya.
5. Kumbuka kuchagua mayai ya kuatamiza kama ilivyoelekezwa ili kuepuka kupata mayai viza.
6. Vifaranga wadogo hadi wiki 8 huhitaji matunzo mazuri fuata maelekezo kuzuia vifo.
7. Kumbuka ukiuza kuku wengi kwa mpigo utaongeza mapato yako, jitahidi kuzalisha vifaranga kwa wingi ili upate kuku wengi baadaye.
8. Muone mtaalamu wa mifugo uliyekaribu naye kwa ushauri zaidi.
9. Soma maelekezo haya mara kwa mara na ufanye yaliyoelekezwa.
10. Washirikishe wengine katika kaya yako ili nao wajifunze na kufanya, hivyo kukuza ufugaji na kipato cha familia.

Imetolewa na Mradi wa Uboreshaji Maisha kupitia Elimu ya Ufugaji Bora wa Kuku wa Asili wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa Ufadhili wa Wellcome Trust ya Uingereza.